# UFUGAJI BORA WA SUNGURA

**Kimetungwa na:**

**G.H. Laswai**
**B.V. Mnembuka**
**S.C. Lugeye**

**Na Kuhaririwa na:**

**Miraji Ngetti**

**2000**

**SUA-TU LINKAGE PROJECT**

# UFUGAJI BORA WA SUNGURA

## YALIYOMO


1. Utangulizi ..........................................................................
2. Faida za Ufugaji wa Sungura ...........................................
3. Aina za Sungura ..................................................................
4. Lishe na Ulishaji wa Sungura............................................
5. Namna ya Uchanganyaji wa
   Chakula cha Sungura...........................................................
6. Namna ya kulisha sungura ..................................................
7. Nyumba ya Sungura ............................................................
8. Vifaa vya kufugia Sungura...................................................
9. Kuzalisha Sungura...............................................................
10. Matatizo ya Ufugaji wa Sungura..........................................
11. Afya ya Sungura ..................................................................
12. Kuweka kumbukumbu .........................................................
13. Kumshika na kumbeba Sungura..........................................
14. Kumchinja na kumtayarisha Sungura ...............................

## 1. Utangulizi

Kijitabu hiki kimetayarishwa ili kukidhi mahitaji ya wafugaji wa sungura katika nchi yetu. Kitajihusisha zaidi na kanuni muhimu ambazo mfugaji wa sungura anapashwa kuzifuata au kuzingatia wakati akitunza wanyama hawa.

Sungura ni mnyama mdogo ambaye ni rahisi kufuga kwa watu wengi. Mnyama huyu anaweza kusaidia katika kuondoa tatizo la uhaba wa nyama katika sehemu nyingi hapa nchini.

## 2. Faida za Ufugaji wa Sungura

Zifuatazo ni faida za kufuga sungura

(a) Urahisi wa kulisha sungura:
Wanyama hawa wanaweza kulishwa masalia ya vyakula vya nyumbani kama: kabeji, mihogo, majani ya aina mbalimbali na hata magugu yatokayo mashambani. Kadhalika, sungura wanaweza kulishwa vyakula ambavyo haviliwi na binadamu. Ili wakue haraka inashauriwa sungura wapewe kiasi kidogo cha pumba au unga wa nafaka.

(b) Chakula kidogo bali nyama nyingi:

Sungura ana uwezo wa kutumia chakula kidogo na kutoa nyama nyingi.

(c) Huzaliana haraka:

Sungura wanaweza kuzaa mara 4-5 kwa mwaka, watoto 6-8 kwa mzao mmoja. Kwa njia hii sungura jike linaweza kutoa sungura 25-35 kwa mwaka. Pia sungura 3 wanaweza kutosheleza nyama kwa familia moja kwa juma.

(d) Hukua haraka:

Sungura hukua haraka kama kuku wa nyama na wanaweza kuchinjwa baada ya majuma 8 wakiwa na uzito wa kilo 2.

(e) Nyama nyingi na nzuri:

Asilimia 93 ya nyama ya sungura inalika kwani ina mifupa na mafuta kidogo. Nyama ya sungura ina madini ya chokaa (calcium), chuma (iron) na vitamini. Nyama ya sungura pia ni bora sana kwa watu wenye matatizo ya moyo.

(f) Mnyama mdogo:

Udogo wa sungura unarahisisha kumhudumia kwani hata watoto wadogo ni rahisi kufuga.

Sungura anahitaji sehemu ndogo ya kumfugia. Sungura anaweza kuchinjwa na kuliwa katika mlo mmoja na hii huondoa tatizo la utunzaji wa nyama.

(g) Mazao mengine:

Mbolea ya kinyesi cha sungura ni nzuri kwenye bustani na mashambani kwa sababu ina madini aina ya "nitrogen" na "phosphorus" ambayo yanahitajika kwenye mimea. Ngozi ya sungura inaweza kutumiwa kutengenezea vifaa mbalimbali kama makoti, mikeka, na mapambo ya ukutani.

## 3. Aina za Sungura

Sungura wapo wa aina nyingi. Unapochagua aina ya sungura mambo yafuatayo hayana budi kuzingatiwa:

(a) Uwezo wa kutoa nyama nyingi
(b) Uwezo wa kuzaa watoto wengi
(c) Uwezo wa kukuza vitoto vingi

Aina za sungura wanaopatikana Tanzania ni kama ifuatavyo:

(a) New Zealand white:

Ni sungura mkumbwa, mweupe mwenye macho mekundu. Sungura huyu ana nyama nyingi na huzaa watoto wengi.

(b) California:

Ni sungura mweupe mwenye mabaka meusi puani, masikioni, miguuni na kwenye mkia. Sungura huyu ana nyama nyingi na huzaa watoto wengi.

(c) Chinchilla:

Sungura huyu ana rangi ya kahawia na ana ukanda wa rangi nyeusi kwenye uti wa mgongo. Sungura wa jamii hii wana nyama nyingi na huzaa watoto wengi.

(d) Dutch:

Kuna aina sita maarufu katika jamii hii ya sungura yaani, kahawia, nyeusi, bluu, kobe, rangi ya chuma na kijivu. Sungura hawa ni shupavu, wenye mwili mdogo na nyama ya wastani. Sungura wa aina hii hutumika sana katika maabara kwa utafiti kwa sababu ya mwili kuwa mdogo.

(e) Sungura wa Polish

Sungura hawa ni wadogo na wenye rangi nyeusi na kijivu. Sungura hawa wana mwili mdogo na nyama kidogo.

(f) Sungura mchanganyiko

Sungura hawa wanapatikana baada ya kuchanganya damu kati ya sungura waliotajwa hapo juu.

## 4. Lishe na Ulishaji wa Sungura:

Ufugaji wa sungura wazuri na wenye afya ni ule unaozingatia chakula ambacho kinatimiza mahitaji ya mwili wa sungura. Wanaweza kulishwa mabaki ya chakula yakiwa bado hayajaoza, pia kulishwa majani na mabaki ya mashambani. Iwapo sungura watalishwa majani peke yake, wanyama hawa watahitaji kula kiasi kikubwa sana ili kufikia mahitaji yao. Chakula cha majani peke yake huwafanya kutofikia mahitaji na hivyo hukua taratibu. Sungura wanaweza kulishwa vyakula vinavyouzwa kwa ajili ya kuku na vikichanganywa na majani huwafanya sungura kukua haraka. Jambo la kuzingatia ni kuhakikisha kwamba sungura anapata vyakula vinavyompatia:

(a) Nguvu:

Hivi ni vyakula vya aina ya nafaka kama vile mahindi, mtama, uwele, pumba za mahindi au mpunga. Mizizi ya mimea kama mihogo pia hutumika.

(b) Protini:

Vyakula vya aina ya protini ya mimea na ya wanyama vinahitajika kwa kujenga mwili wa sungura. Vyakula hivi ni kama vile aina ya maharage, mashudu na dagaa.

(c) Madini na vitamini:

Vyakula vyote vina kiasi fulani cha madini na vitamini, lakini mboga za majani au majani mabichi hutosheleza zaidi.

(d) Aina ya nyasi:

Aina hii ya chakula inafanya chakula kusagika vyema tumboni na kuzuia kuhara kwa sungura. Vyakula hivi vyote vikichanganywa kwa kiasi maalum humpatia sungura mahitaji yake ya mwili.

## 5. Namna ya Uchanganyaji wa Chakula cha Sungura

Jitihada lazima ifanywe katika kutumia vyakula vinavyopatikana kwa urahisi katika mazingira ya mfugaji na ambavyo vitakidhi mahitaji ya sungura.

### 5.1 Mifano ya uchanganyaji wa chakula

| Orodha ya vyakula vinavyoweza kutumika | Kiasi cha kutumia (kg) | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Mfano Na. 1 | Mfano Na. 2 | Mfano Na. 3 | Mfano Na. 4 |
| Mihogo | 24 | - | - | - |
| Pumba za mpunga | 25 | 25 | - | 20 |
| Uwele | 10 | - | - | - |
| Mashudu | 21.5 | 26 | 25 | 14 |
| Dagaa | 18 | 18 | 18 | 15 |
| Mahidi | - | 20 | - | 25 |
| Mtama | - | 10 | 15 | - |
| Pumba za mahindi | - | - | 32 | - |
| Luceana | - | - | - | 10 |
| Chunga | - | - | - | 15 |
| Chumvi | 0.5 | 0.5 | 0.5 | 1.0 |
| Chokaa | 1 | 0.5 | 0.5 | - |
| | 100 | 100 | 100 | 100 |

Uwekapo majani mengi kwenye chakula, sungura atapaswa kutumia chakula kingi zaidi ili kujitosheleza mahitaji yake ya mwili.

Sungura wapewe chakula cha kutosha na kamili ili wafikie uzito unaohitajika haraka. Aidha, huwasaidia kustahimili maradhi. Sungura anayelishwa vyakula vya gharama nafuu vipatikanavyo vijijini anakuwa taratibu lakini gharama ya uzalishaji zinakuwa ndogo.

## 6. Namna ya kulisha Sungura

Hakikisha kuwa vifaa vya kulishia sungura ni safi. Sungura wadogo wanaozidi umri wa majuma manane na kupungua majuma ishirini wapewe kiasi cha kikombe kimoja cha chai (gramu 300) cha chakula kilichochanganywa kwa kila sungura wawili kwa siku. Sungura wenye mimba na wanaonyonyesha hakikisha kwamba kwenye vyombo vyao vya chakula, kuna chakula wakati wote ili wale kama wapendavyo.


Sungura madume na majike ambayo hayana mimba wala hayanyonyeshi yapewe theluthi moja ya kikombe cha chai (gramu 100) ya chakula kilichochanganywa kwa siku. Sungura wa


aina zote wapewe majani mabichi kwa wingi. Sungura wanaweza kupewa masalia ya chakula pamoja na vyakula vinginevyo wanavyopenda wakati wowote.

## 7. Nyumba ya Sungura

Miongoni mwa vitu muhimu vya kuzingatia katika ufugaji wa sungura ni ujenzi wa nyumba imara, ili iwakinge dhidi ya joto kali, baridi, mvua, na upepo mkali. Aidha lazima nyumba iwakinge na maadui kama paka, mbwa, nyoka, siafu, panya na wanyama wengine wa porini. Ili kuzuia wizi, nyumba ya sungura lazima ifungwe madhubuti. La muhimu pia katika ujenzi wa nyumba ya sungura ni matumizi ya nyenzo zinazopatikana kwa gharama nafuu katika mazingira ya mfugaji mwenyewe. Sungura huathiriwa na joto kali hasa katika uwezo wa kizazi, hamu ya kula chakula na hata kusababisha vifo.

Sakafu ya nyumba ya sungura ingefaa iinuliwe juu ya ardhi ili kuwezesha kinyesi na mkojo kupita kwa urahisi hadi ardhini na hivyo kuifanya nyumba ya sungura kuwa kavu na nadhifu daima (ona michoro ifuatayo).






Nyumba ya sungura ni vizuri ijengwe mahali palipoinuka kidogo ili kuepuka tatizo la kutuama kwa maji. Nyumba ingefaa ijengwe ikiwa na kuta ndefu zikielekea mashariki-magharibi. Hii itafanya nyumba ya sungura isipigwe na miali ya jua moja kwa moja hasa saa za mchana.

Kuwepo kwa miti ya vivuli karibu na nyumba ya sungura ni jambo la kusisitizwa. Nyumba ya sungura ni vizuri ijengwe karibu na maskani ya mfugaji kwa usalama zaidi.

Hata hivyo ni vizuri nyumba hiyo itengwe na sehemu zenye kelele na mishituko mbali mbali ambayo inaweza kuwaogofya sungura.

Katika ujenzi wa nyumba ya sungura, mfugaji ingefaa ailewe hali ya hewa ya mahali anapoishi kama hali ya joto, mvua, mwelekeo na kasi ya upepo, mwanga, na baridi n.k. Hivi vitamsaidia kuchagua aina za nyumba zitakazowafaa sungura wake.

## 8. Vifaa vya Kufugia Sungura

Vifaa muhimu katika ufugaji wa sungura ni pamoja na vinywesheo, vilishio na visanduku vya kuzalia.

Vinywesheo vinaweza kuwa vyupa, makopo au vyombo vya udongo. La muhimu kwa vyombo hivi ni kwamba visafishike kwa urahisi, visiwe vipana mno kiasi cha sungura kudumbukia; aidha visiwe vidogo mno kiasi cha kumfanya sungura ashindwe kunywa maji. Hatimaye ni lazima vifungike au viwe vizito kiasi cha kuhakikisha kuwa havianguki na kumwaga maji.

Vilishio vinaweza kuwa makopo, visanduku vya mbao, vyombo vya udongo na vihori vya waya kwa ajili ya

majani. Ni vizuri hivi viwekwe kati ya visanduku vya kufugia. Sifa za vifaa hivi ni kama zile za vinywesheo.

Visanduku vya kuzalia vinaweza kutengenezwa kwa mbao. Debe pia laweza kutumika. Visanduku hivi lazima viwe na ukubwa wa kutosha kiasi cha 12" x 12" x 16". Aidha lazima viwe na giza la kutosha au vipakwe rangi nyeusi ndani ili kupunguza mwanga la sivyo jike litavitupa vitoto. Visanduku hivi viwekwe majani laini siku tano kabla ya siku ya kuzaa kwa jike.



9. **Kuzalisha Sungura**

(a) **Mambo muhimu ya kuzingatia katika kuchagua** sungura wa kuzalisha ni yafuatayo:

(1) Chagua sungura wakiwa na umri wa miezi 2-5 na wafikiapo umri wa miezi 6-7 ndipo wapandishwe.

(2) Chagua wanyama wenye rangi na siyo weupe. Sungura weupe wanapendwa tu kama ni kwa uzalishaji wa ngozi, kwani ngozi ya sungura weupe zina bei zaidi.

(3) Chagua sungura wenye manyoya mafupi. Hawa wanastamili joto kuliko wenye manyoya marefu.

(4) Chagua sungura kutoka kwenye familia zenye historia ya kuwa na vitoto vingi kwa mzao mmoja na zinazoweza kuvilea vitoto hivyo.

(5) Chagua wanyama ambao hawana magonjwa ya ngozi, vidonda au vilema.

(6) Hakikisha kuwa madume yanayochaguliwa yana kende zote mbili na zinaonekana.

(b) Mpango wa kuzalisha

Sungura jike lazima liwe na umri wa miezi 7 na dume miezi 7-8 kabla ya kupandishwa mara ya kwanza. Sungura ambaye ana umri wa zaidi ya miaka mitatu asitumiwe tena kuendeleza kizazi. Sungura ambao wana uhusiano wa karibu, kama baba na binti, dada na

kaka, n.k. wasitumike katika uzalishaji kwa vile husababisha kuzaliwa vitoto vilema na pia hupunguza uzazi.

Sungura dume moja linahitajika kwa majike kumi na linaweza kutumiwa kupanda majike 2-3 kwa juma moja. Kutumia dume kupanda majike mengi zaidi kunapunguza uzazi. Kwa hali ya kijijini jike linaweza kuzaa mara nne kwa mwaka na kila mzao kutoa vitoto 5-8. Majike yatoayo vitoto 2-3 mara mbili mfululizo yatapaswa kuondolewa kwenye kundi.

(c) Kupandisha

Sungura jike linaweza kupandishwa wakati wowote na likapata mimba. Daima jike lipelekwe kwa dume wakati wa kupandisha sungura. Dume likipelekwa kwa jike, ugomvi unaweza kutokea. Dume likshapanda, kwa kawaida huanguka kiupande na kutoa sauti kuonyesha kufanikiwa katika upandaji wake. Kama upandaji haukufanikiwa, rudisha jike kwake na kulirudishia tena baada ya siku chache. Kama jike halikubali kwa urahisi kupandwa, liachwe hapo kwa siku moja. Nyakati nzuri za kupandisha ni asubuhi na jioni kukingali na hali ya ubaridi.

(d) Mimba

Kwa kawaida majike hukaguliwa kama yana mimba siku 14-18 baada ya kupandwa. Hii hufanyika kwa kubonyeza kidogo kwenye tumbo la sungura. Kwa jike lenye mimba, vitu mithili ya gololi vinaweza kuguswa ndani ya hilo tumbo. Sungura huzaa siku 29-31 baada ya kupandishwa. Wakati wa kulea mimba, sungura hana budi kupatiwa chakula kingi na kamili, asisumbuliwe wala kuogopeshwa, anahitaji sehemu yenye ukimywa na safi. Juma moja kabla ya kuzaa sungura jike liwekewe kisanduku cha kuzalia kilichotandazwa nyasi nyingi na laini.

Muda mfupi kabla ya kuzaa, sungura jike hujinyonyoa manyoya kwenye mwili wake na kutayarisha kiota ndani ya kisanduku cha kuzalia. Wakati mwingine jike linaweza kukataa kutumia kisanduku cha kuzalia na hivyo kuzalia popote. Linaweza pia kukataa kuvinyonyesha vitoto vyake. Hii mara nyingi hutokea kama jike linasumbuliwa wakati wa kuzaa au mara tu baada ya kuzaa. Inawezekana kutokea pia kama jike limehamishwa muda mfupi kabla ya kuzaa. Sungura mara nyingi huzaa usiku hivyo tahadhari inabidi ichukuliwe. Vitoto visichezewe au kushikwa kwani

hali hiyo inaweza kusababisha sungura jike kukataa kuvinyonyesha na hata kuvikataa kabisa vitoto vyake. Vitoto vya sungura huzaliwa bila manyoya na macho yamefunga. Macho hufunguka baada ya siku 10-12. Wakati huu pia vinaanza kuota manyoya . Vitoto vinaweza kutolewa kwenye visanduku baada ya siku 19-20. Kabla ya hapo, hakikisha kuwa vitoto havitoki nje ya visanduku visije vikafa kwa baridi (kwa nyakati za baridi) au kuachwa bila kunyonyeshwa.

Ni muhimu pia kuhakikisha kuwa nyumba haina matundu makubwa ambamo vitoto vinaweza kupenya na kuweza kuchukuliwa na maadui.

(e) Vitoto lazima viangaliwe mara kwa mara kama kuna vilivyokufa au vyenye vilema viondolewe. Chakula kisiwekwe ndani ya kiota kwani kitavutia maadui, kama panya.

## 10. Afya ya Sungura

Usafi wa mazingira ya wanyama huzuia uwezekano wa kutokea magonjwa. Ili kudumisha afya ya sungura yafuatayo inabidi yazingatiwe:

(a) kuondoa mabaki ya vyakula na maji na kusafisha vyombo kila siku.

(b) kuondoa vyumbani majani yaliyoloa na mbolea.

(c) kutenganisha wanyama wagonjwa na wazima.

(d) wanyama wageni wasichanganywe kwenye kundi, ila watengwe angalau kwa majuma mawili.

Yafuatayo ni baadhi ya matatizo na magonjwa ya sungura:

(a) Miguu yenye vidonda
Sungura hushindwa kutembea sawasawa na hamu ya chakula kupungua. Ili kuepuka tatizo hili hakikisha sakafu ni salama na haina ncha kali au misumari.

(b) Ugonjwa wa ngozi
Husababishwa na funza ambao hutaga mayai kwenye ngozi. Husababisha kujikuna, manyoya kupotea na kuleta maumivu. Usafi na kuepuka vumbi kwenye nyumba hupunguza tatizo hili.

(c) Kuhara damu

Sungura hutoa kinyesi laini na chenye damu. Hukonda na kukosa damu. Usafi wa nyumba na vifaa vyake husaidia kuzuia ugonjwa huu. Sungura wakubwa na wadogo watenganishwe.

(d) Kujaa tumbo

Ugonjwa huu husababishwa na kula nafaka kwa wingi. Punguza nafaka na lisha majani kwa wingi.

(e) Ugonjwa wa meno

Huu ni ugonjwa wa kurithi, ambapo meno ya mbele hurefuka kupita kiasi. Ugonjwa huu hautibiki, hivyo sungura atolewe kwenye kundi na kuchinjwa.

(f) Kuhara (coccidiosis)

Sungura huharisha, kutokula chakula, tumbo kuvimba na manyoya husimama. Mara nyingine damu huonekana kwenye kinyesi. Chakula na vibanda vichafu husababisha ugonjwa huu. Vibanda na vifaa vyote visafishwe. Matumizi ya wavu kama sakafu hupunguza tatizo hili. Dawa ya aina ya "sulphanezathine 16%" yaweza kuwekwa kwenye maji ya kunywa na kupewa sungura wote.

(g) Vidonda vya masikio

Masikio huwasha na kufanya sungura ajikune au kutikisa kichwa. Hii husababishwa na utitiri. Masikio ya sungura yasafishwe kwa kutumia pamba. Dawa ya "Benzyl Benzoate" yaweza kuwekwa sehemu zilizodhurika.

(h) Vichomi

Joto la mwili la sungura hupanda, naye huhema na kukohoa. Unyevunyevu na upepo wa baridi kwenye nyumba na pia kulowana manyoya ya sungura huweza kusababisha ugonjwa huu.

(i) Baridi

Zuia upepo kwenye nyumba ya sungura. Ubaridi unaweza kusababisha vifo hasa kwa vitoto. Kama kuna baridi au unyevu funika kuta au tengeneza visanduku vidogo.

## 11. Kuweka kumbukumbu

Uwekaji wa kumbukumbu ni utaratibu unaowezesha kufuatilia uzalishaji wa sungura. Ni rahisi kufuatilia tarehe za kupandwa na za kuzaa, kutenganisha vitoto, kuchagua wazazi na kuondoa sungura waliozeeka. Sungura wote wanaotumika kama wazazi inabidi wawe na namba.

Kumbukumbu muhimu katika ufugaji wa sungura ni kama zifuatavyo:

(a) Kumbukumbu za uzalishaji

Sungura ....................................

Tarehe ya kupandisha ..............................

Tarehe ya kuzaa .......................................

Idadi ya watoto waliozaliwa .............................

(b) Kumbukumbu ya uzazi kwa jike

Jina .................................................

Jike ...................................................

Tarehe ya kuzaliwa.........................................

Baba ............................. mama ............................

| Tarehe ya kupandisha | Dume | Tarehe ya kuzaa | Jumla ya watoto | | Tarehe ya kute-nganisha | Jumla yao |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Hai | Wafu | | |
| | | | | | | |

(c) Kumbukumbu ya uzazi kwa dume

Aina ........................................................

Dume ......................................................

Tarehe ya kuzaliwa ..................................

Mama ..........................................

Baba ...........................................

| Jike alilopanda | Tarehe ya kupanda | Amezaa | | Hakuzaa | Walioteganisha |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Hai | Waliokufa | | |
| | | | | | |

## 12. Kumshika na Kumbeba Sungura

Viungo vya sungura ni vidhaifu. Sungura wasinyanyuliwe kwa kushikwa masikio au miguu. Njia nzuri ni kuwashika katika sehemu ya kiunoni na hatimaye akumbatiwe katika kwapa akiwa amelalia tumbo lake juu ya mkono wa mbebaji.

Sungura wakubwa zaidi na wazito wanaweza kubebwa kwa kufumbatwa kwapani na hali wamelalia migongo yao juu ya mkono wa mbebaji.

## 13. Kuchinja na Kutengeneza Sungura

Katika kumchinja sungura lengo liwe ni kuwa mnyama auawe kwa haraka bila maumivu ya muda mrefu. Baada ya hapo sungura aning'inizwe kwa kutumia miguu ya nyuma na kuchunwa kama ifuatavyo:

(a) Kata ngozi kwenye kila mguu mpaka kwenye tuzi halafu mpaka shingoni.


(b) Kata kichwa na miguu ya mbele.

(c) Vuta ngozi mpaka mapajani.

(d) Geuza mnyama na kata ngozi sehemu ya kiunoni.

(e) Vuta ngozi yote hadi miguu ya mbele.

Ukishachuna, pasua tumboni na kifuani kisha toa utumbo, mapupu kifuani na koromeo. Kata miguu ya nyuma na safisha kwenye maji mengi.

Kwa ladha nzuri, nyama ya sungura ikaangwe au kubanikwa na kuongeza viungo kadri ya matakwa ya mlaji.